

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA TANO**

**12 APRILI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA TANO – TAREHE 12 APRILI, 2023**

#### I. DUA:

#### II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:

#### WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na.05 la tarehe 03 Februari, 2023;
2. Toleo Na.06 la tarehe 10 Februari, 2023;
3. Toleo Na.07 la tarehe 17 Februari, 2023;
4. Toleo Na.08 la tarehe 24 Februari, 2023;
5. Toleo Na.09 la tarehe 03 Machi, 2023;
6. Toleo Na.10 la tarehe 10 Machi, 2023;
7. Toleo Na.11 la tarehe 17 Machi, 2023;
8. Toleo Na.12 la tarehe 24 Machi, 2023; na
9. Toleo Na.13 la tarehe 31 Machi, 2023.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **53. MHESHIMIWA EDWARD OLELEKAITA KISAU (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itawaajiri Walimu wanaojitolea katika Jimbo la Kiteto.

##### **54. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka Watumishi na Vifaa Tiba katika Kituo cha Afya Majengo.

##### **55. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga majengo ya kisasa katika Vituo vya Afya vya Kinyangira na Mkalama katika Halmashauri ya Mkalama.

## **OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

### **56. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya upungufu wa Watumishi katika Mkoa wa Katavi.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **57. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Masasi – Nachingwea kwa kiwango cha lami.

### **58. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya kutoka njia panda ya Iyula – Idiwili - Nyimbili hadi lleje itajengwa kwa kiwango cha lami.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **59. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti matukio ya ubakaji na Ulawiti katika Shule za Bweni.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **60. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo kipyaa cha Polisi cha Wilaya Micheweni pamoja na kupeleka Samani.

## **WIZARA YA AFYA:**

### **61. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itaongeza Watumishi wa Afya katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**62. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiongezea mtaji kiwanda cha Kahawa cha TANICA.

**WIZARA YA KILIMO:**

**63. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia Wakulima wa Tarime wanaolima Kahawa aina ya Arabika.

**WIZARA YA MAJI:**

**64. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa maji Kabanga.

**65. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itajenga chujio la kuchuja na kutibu maji toka chanzo cha maji Nyamtukuza kabla ya kuyapeleka kwa Wananchi.

**WIZARA YA MADINI:**

**66. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha Wanawake wanashiriki kikamilifu kwenye mnyororo wa Madini.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**67. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itabadili majina ya Kigeni kuwa ya Kitanzania kwenye Rasilimali za Taifa ikiwemo Mlima Livingstone na Ziwa Victoria.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

##### **WAZIRI MKUU:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA**  
**12 APRILI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**

